

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
WAKALA WA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO



**KICHA
CHA
MBWA**

Kimetayarishwa na:

Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)
Kampasi ya Morogoro
S.L.P. 603,
MOROGORO – TANZANIA
E-mail: litamorocamp@gmail.com

UTANGULIZI

Kichaa cha mbwa ni ungonjwa hatari kwa binadamu na wanyama wafugwao na wa porini. Ugonjwa huu hauna tiba na umeenea karibu nchi nzima ya Tanzania.

HUSABABISHWA NA NINI?

Kichaa cha mbwa husababishwa na virusi ambavyo hukaa na kuzaliana kwenye mishipa ya fahamu, ubongo na uti wa mgongo na baadaye huenea kwenye maji maji hasa mate.

AINA MBILI ZA KICHAZA CHA MBWA

- Kichaa cha mbwa ambacho huenezwa na mbwa wafugwao.
- Kichaa ambacho huenezwa zaidi na wanyama pori kama vile mbweha, fisi na mbwa mwitu.

NANI HUPATA UGONJWA HUU

Kichaa cha mbwa huwapata binadamu, wanyama wote wenye damu joto, wafugwao na kama vile mbwa, paka, ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, farasi na punda. Wanyama pori na kama vile mbweha, fisi na paka mwitu.

HUENEAJE:

Kwa kuumwa na wanyama wenye virusi vya ugonjwa.

- Kwa kugusana na mate, machozi, maziwa au maji maji yenye virusi kuitia kidonda na michubuko.

DALILI ZA KICHAZA CHA MBWA

Dalili huonekana baada ya wiki mbili hadi miezi sita, kutegemeana na umbali kati ya ubongo na mahali virusi vilipoingilia. Dalili zimegawanyika katika hatua kuu tatu lakini si lazima mnyama aonyeshe dalili katika hatua zote tatu. Dalili hizo ni:

1. Kubadilika tabia

Hatua hii hujitokeza baada ya siku tatu na dalili zake ni; Mnyama hubadilika tabia

- Mnyama mkimya anakuwa mkali
- Hujitenga na kukaa peke yake
- Wanyama pori huweza kuchanganyika na binadamu bila woga.

2. Kuwa na hasira:

Hatua hii huonekana baada ya majuma mawili tangu mnyama kupata ugonjwa. Dalili zake ni:

- Mnyama hugonganisha meno.
- Kubweka ovyo
- Kuogopa mwanga na kujificha
- Kuuma ovyo au chochote kilichokaribu yake
- Hatua hii huchukua siku moja hadi nane.

3. Kupooza:

- Mnyama hypooza mwili
- Huacha kula
- Huwa dhaifu
- Hutokwa mate mengi na kushindwa kufunga mdomo
- Miguu ya nyuma na mkia hufa ganzi na kukosa fahamu
- Mwisho mnyama huanguka chini, hushindwa kusimama na kufa
- Hatua hii huchukua siku moja hadi nne.

KICHAZA CHA MBWA KWA BINADAMU

Binadamu hupata kichaa kuanzia siku ya 14 hadi miezi 6 mpaka 12 baada ya kuumwa, kutegemea umbali wa jeraha kutoka kichwani. Mara nyingi hupata kichaa wakati jeraha limeshapona.

- Dalili za kupooza misuli, kushituka, kuchanganyikiwa na kupoteza fahamu hujitokeza
- Huogopa kunywa maji anapokuwa na kiu
- Huendelea kupooza hadi kifo.

JE NIKIUMWA NA MBWA NIFANYEJE?

- Kamua damu kwenye jeraha ili kutoa vimelea
- Safisha jeraha kwa maji mengi na sabuni au dawa ya kuulia vimelea
- Nenda hospitali mara moja upate chanjo ya kuzuia kichaa cha mbwa na matibabu.
- Toa taarifa kwa mganga wa mifugo aliye karibu nawe mara moja.

KINGA

- Kinga pekee ya kichaa cha mbwa ni chanjo
- Chanja mbwa na paka kila mwaka kuzuia kichaa cha mbwa
- Wanyama wadogo wachanjwe baada ya umri wa miezi mitatu na chanjo irudiwe baada ya mwaka mmoja
- Chanjo hufanywa na wataalamu tu ili kuzuia udanganyifu.
- Wananchi wazingatie karantini,
- Wawajengee mbwa vibanda vyta kuwafunga mchana ili wasizurure ovyo
- Kuwaua mbwa wagonjwa na wazururaji
- Kudhibiti usafirishaji wa mbwa na paka nje na ndani ya nchi
- Wanyama pori wapewe chanjo.